TANGAZO LA SERIKALI Na.176 la Tarehe 8/3/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA( MAMLAKA ZA MIJI)

SURA YA 288

---

## SHERIA NDOGO

---

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89*

---

SHERIA NDOGO ZA ( UTAMADUNI  NAVIBALI VYA BURUDANI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA  ZA MWAKA, 2019

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Utamaduni na Vibali vya Burudani) za  Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga za Mwaka,2019 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga;

Tafsiri

"ada"  maana yake ni kiwango cha fedha kitakachopangwa na Halmashauri na kutozwa katika shughuli za burudani yoyote isipokuwa ile ya kiserikali au  madhehebu ya kidini;

"Afisa Mwidhiniwa maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji  wa Sheria Ndogo hizi;

"burudani" maana yake ni shughuli yeyote ya kijamii au tukio ambalo litakuwa linafanyika kwa kukusanya watu mbalimbali katika ukumbi au eneo lolote la wazi au viwanja litakalolipiwa kibali Halmashauri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya

Sumbawanga ;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"sherehe" ina maanisha mkusanyiko wa watu unaoenda na shamrashamra katika ukumbi, mtaa, uwanja au eneo lolote litakaloruhusiwa na Halmashauri;

"ukumbi wa video" maana yake ni jengo lolote lililoidhinishwa na Halmashauri kwa shughuli za kuonesha video;

"video na sinema" maana yake ni picha zozote zinazooneshwa katika kumbi za video na sinema zenye maadili mema;

Kibali

4.-(1) Mtu yoyote au taasisi yeyote isiyokuwa ya kiserikali au kidini itakayotaka kuendesha shughuli za burudani, watalazimika kuomba kibali cha kuendesha shughuli hiyo kutoka Halmashauri kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kibali hicho kitalipiwa ada kama iliyooneshwa katika Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Mwaka, 2018.

(3) Kibali hicho kitaonesha;-

(a) sehemu itakayofanyika shughuli hiyo;

(b) muda wa kuanza na kumalizika kwa shughuli hiyo; na

(c) aina ya shughuli au burudani

(4) Nakala ya kibali hicho itapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ikiwa na viambatanisho vyote husika.

Marufuku

5.-(1) Ni marufuku kwa mwenye ukumbi wa video na sinema au sehemu yoyote kuonyesha picha za video ambazo hazina maadili.

(2) Ni marufuku kwa wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) kuingia katika kumbi za burudani au muziki.

Wajibu

6.-(1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa ukumbi wa muziki kupiga muziki kwa kiwango cha sauti cha kawaida bila kuathiri watu wanaozunguka eneo la ukumbi huo wa muziki.

(2) Kila mwonesha video au sinema atatakiwa kuweka sauti ya chini wakati wa onyesho bila kuathiri majirani wanaomzunguka.

(3) Ni wajibu wa kila mmiliki wa kumbi za burudani au baa au muziki kuhakikisha wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) haruhusiwi katika kumbih izo na endapo itabainika kuingia kwa wanafunzi au watoto hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mmiliki wa kumbi hizo.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

7. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika ukumbi wowote wa burudani, sinema au sherehe yeyote inayofanyika mtaani na hadharani kukagua kibali kinachoruhusu uendeshaji wa shughuli hiyo.

Kibali Maalum

8. Mtu au kikundi chochote kitakachofanya sherehe katika mitaa au viwanja vya wazi atapaswa aombe kibali cha kufunga barabara ya Mtaa au kiwanja atakachofanya skeche hiyo.

Muda wa Burudani

9.-(1) Muda wa kuonyesha video au sinema utakua ni siku ya jumamosi na jumapili kuanzia saa saba (7) mchana hadi saa kumi na mbili (12) jioni;

Makosa

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote endapo;

(a) Atapiga muziki unaosababisha kero kwa majirani;

(b) Atafanya sherehe yeyote bila kupata kibali;

Adhabu

10. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo..

**JEDWALI**

*(Limetungwa Chini ya kifungu cha 4 (1))*

**FOMU YA MAOMBI YA KIBALI**

**SEHEMU YA KWANZA (Taarifa za Mwombaji)**

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mwombaji au  Kampuni; ……………..…………………………. | 2. Anwani ya Mwombaji; ……………………….……………………… |
| 3. Aina ya Shughuli; ……………….……..... | 4. Eneo analokusudia kufanya shughuli ………………………………………………… |
| 5. Muda wa kuanza ; ……………………………………….. | 6. Muda wa kumaliza …………………………………………… |

| | |
|---|---|
| . | |
| 7. Ada ya kibali Tsh. …………………........... | 8. Stakabadhi ya malipo; ……………………… |
| Saini: ……………………………………….<br>Tarehe: …………………………………….. | |

**SEHEMU YA PILI (Kwa Matumizi ya Ofisi)**

| | |
|---|---|
| 1. Maombi Na.……………..……..……… | 2. Ada ya kibali Sh:. …………........... |
| 3. Namba ya Stakabadhi ya malipo: ……….. | 4. Tarehe:…………………………….. |

**Maoni ya Afisa Mwidhiniwa**: - *Nakubali/Sikubali (*weka alama ya tiki kwa inayohusika*)

Sababu:

………………………………………………………………………..………………………
……

Jina: ……………………………….………… Saini:

……………………..……………………… Tarehe: ……………………........…

Mwezi............................................ Mwaka.................................

*Tangazo la Serikali Na. 176 (linaendelea)*

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 2 ya mwezi Septemba, mwaka 2018. Nembo imebandikwa mbele ya:

JACOB J. MTALITINYA
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Sumbawanga*

JASTIN E. MALISAWA
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Sumbawanga*

NAKUBALI

Dodoma,
11 Februari, 2019 `

SELEMANI S. JAFO
*WN-OR-Tamisemi*